NAIROBI

## Kananu kuapishwa kumrithi Mike Sonko

**NAIROBI** itapata Gavana mpya baada ya Mahakama ya Rufaa kuamuru aapishwe mara moja kwa Naibu Gavana Anne Kananu.

Wakiamuru Bi Kananu achukue hatamu za uongozi wa Kaunti ya Nairobi, majaji Wanjiru Karanja, Jamila Mohammed na Jessie Lesiit walisema suala la kuapishwa kwake halikulalamikiwa katika mahakama kuu na mwanaharakati Okiya Omtata. Bi Kananu aliyekuwa ameteuliwa Naibu wa Gavana Mike Sonko alikabiliwa na changamoto pale Jaji Antony Mrima alipoamuru asitwae hatamu za uongozi. Jaji Mrima alihoji uhalali wa Bw Sonko kumteua Bi Kananu.

Kuapishwa kwa Bi Kananu kulipingwa na majaji hao watatu wakisema, "suala la kuapishwa halikuwa mojawapo ya tetezi za rufaa hiyo" Bw Omtatah na Bw Sonko waliwasilisha kesi ya kupinga kuapishwa kwa Bi Kananu aliyekuwa ameajiriwa katika idara ya masuala dharura na pia sekta ya maji.

*Na Richard Munguti*

KISUMU

## Naibu wa chifu mbaroni kwa mauaji

**NAIBU** chifu mmoja katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi, anazuiliwa katika Gereza la Kibos kwa tuhuma za kumtesa na kumuua mwanamume mwenye umri wa miaka 32.

Bw Joel Juma Oliewo, ambaye anahudumu katika kata ndogo ya Kadogo alifikishwa mahakamani ambapo alishtakiwa kwa kosa la kumuua Bw Erick Ochieng Atito, akidai alilenga kumtia "adabu" mnamo Oktoba 8, 2021.

Siku ya tukio, ilidaiwa Bw Atito alionekana akitembea na mwanamke mmoja mwendo wa saa tatu unusu usiku. Baadaye mwanamke huyo alipiga kamsa akidai mwanamume huyo alijaribu kumbaka.

Ilidaiwa wananchi walimshambulia marehemu kabla ya Bw Aliewo na maafisa wa polisi kumnusuru na kumpelekea katika kituo cha polisi cha Holo.

*Na Rushdie Oudia*

KWALE

## Bamburi yasifiwa kwa kuokoa elimu ya watoto masikini

**JUHUDI** za kampuni ya kutengeneza saruji, Bamburi Cement, za kutoa ufadhili wa masomo kwa watoto kutoka jamii masikini katika kaunti ya Kwale zilisaidia watoto wote waliokamilisha darasa la nane kujiunga na shule za upili.

Kampuni hiyo ilitoa ufadhiliwa wa masomo wa thamani ya Sh1.1 milioni kupitia mpango wake wa kusaidia jamii.

Wanafunzi waliosalia nyumbani kwa kukosa karo walijawa na furaha Bamburi Cement ilipowapa ufadhili mkamilifu. Afisa Mkuu Sadiq Hassan alisema wanafunzi waliofaidi waliteuliwa kwa kuzingatia walivyofanya katika KCPE.

*Na KNA*

**KILIO CHA HAKI:** Mwili wa Tirop waondolewa mochari




**WANARIADHA, makocha na umma waandamana wakati wa kuondolewa kwa mwili wa mwanariadha Agnes Tirop, katika Mochari ya Eldoret mjini Eldoret, ambaye ni mshindi mara mbili wa medali ya shaba katika mbio za mita 10,000 katika Riadha za Dunia. Tirop anazikwa leo.** *Picha/Jared Nyataya*

### Bei ya bidhaa hiyo imeshuka, NCPB ikiuza yake itapata hasara

# Mahindi ya TZ na UG yaharibu soko Kenya

NAIROBI

Na CHARLES WASONGA

BODI ya Kitaifa ya Nafaka na Mazao (NCPB) imekwama na magunia 700,000 ya mahindi ambayo imeshindwa kuwauzia wasagaji wa nafaka baada ya bei ya zao hilo kushuka huku zaidi ya Wakenya milioni mbili wakikeketwa na njaa inayosababishwa na ukame.

Mwenyekiti wa bodi hiyo, Bw Mutea Iringo amewaambia wabunge kwamba walinunua mahindi hayo mwaka jana wakitarajia kuyauzwa kwa Sh2,700 kila gunia lakini sasa hawawezi kuyauza baada ya soko kujaa mahindi ya bei rahisi kutoka Uganda na Tanzania.

"Tulinunua magunia 700,000 ya mahindi kupitia kitengo chetu cha kibiashara kwa matarajio ya kuyauza kwa faida. Tulitaraji kuyauza kwa Sh2,700 kwa kila gunia la kilo 90 lakini bei imeshuka hadi chini ya Sh2,600 baada ya mahindi mengi kuingizwa nchini kutoka mataifa jirani," Bw Iringo akawaambia wabunge wanachama wa Kamati ya Kilimo mnamo Alhamisi.

Mwenyekiti huyo ambaye alikuwa ameandamana na Afisa Mkuu Mtendaji wa NCPB Joseph Kimote, aliongeza kuwa asasi hiyo inahitaji Sh10 bilioni kutoka kwa serikali ili kuweza kununua magunia milioni 3 ya mahindi ya hifadhi hiyo ya kitaifa.

"Mahindi hayo yatasambazwa kwa wananchi wanaokabiliwa na njaa katika kaunti zilizoko maeneo kame nchini. Wakati huu kitengo chetu cha hifadhi ya kitaifa hakina mahindi," Bw Iringo akaiambia kamati hiyo inayoongozwa na Mbunge wa Moiben, Silas Tiren.

Bw Iringo aliwashangaza wabunge alipodai kuwa mahindi ambayo yanasambazwa na serikali wakati huu, kama chakula cha msaada kwa waathiriwa wa ukame, yanaagizwa na watu binafsi kutoka mataifa jirani.

"Kwa kuwa hatuna mahindi katika kitengo chetu cha hifadhi ya kitaifa, mahindi yanayosambazwa na serikali yanapoagizwa na watu binafsi.

"Hii ni kwa sababu mwaka huu serikali haitaitengea NCPB fedha za kuwezesha kununua mahindi kutoka kwa wakulima," akaeleza.

Lakini wabunge waliwataka wakuu hao wa NCPB kuelezea namna walivyotumia Sh12 bilioni ambazo bodi hiyo ilirithi kutoka kwa Shirika la Hifadhi ya Chakula nchini (SFR) lililovunjiliwa.

"Sh12 bilioni zilizokuwa katika akaunti ya SFR zilienda wapi ilhali baada ya kuvunjiliwa kwake NCPB ndiyo iliyopewa majukumu yake ya kununua mahindi na mazao mengine kwa matumizi nyakati za uhitaji kama sasa?" akauliza Mbunge wa Kiminini Chris Wamalwa. Akijibu, Bw Kimote alisema kuwa pesa hizo zilirejeshwa katika Hazina Kuu.

"Waziri wa Fedha au Katibu katika wizara hiyo ndio wanaoweza kujibu swali hilo. Hii ni kwa sababu pesa zilizokuwa katika akaunti ya SFR zilirejeshwa katika Hazina ya Kitaifa," akaeleza. Wakulima wa mahindi, hasa kutoka eneo la North Rift wamekuwa wakilalama kuwa wanapata hasara baada ya NCPB kufeli kununua mazao yao.

MOMBASA

## Maudhi wizi wa transfoma ukikithiri Pwani

**KAMPUNI** ya Umeme nchini (KP) imelalamikia kukithiri kwa wizi wa transfoma zake Pwani mwa nchi, jambo ambalo limechangia ukosefu au kupotea kwa umeme mara kwa mara na kuwakera wakazi wa eneo hilo.

Meneja wa Ukanda wa Pwani, Hicks Waswa jana alisema kuwa transfoma saba ziliibwa na wateja 1,600 wakakosa umeme. Maeneo ya Kengeleni, Kongowea, Majengo, uga wa Tononoka, ukumbi wa Tononoka, Chaani na Changamwe ndiyo yaliyoathirika.

"Inasikitisha wizi wa transfoma umeongezeka hasa katika kaunti za Mombasa na Kilifi. Huu ni uhalifu ambao hatutauvumilia kamwe," akasema Bw Waswa akiongeza kuwa uharibifu wa transfoma ndio changamoto katika kuwapa wakazi wa Pwani huduma za umeme zinazoaminika. Afisa huyo wa KPC alisema watu wanne wamefikishwa kortini kutokana na wizi huo na kesi zao zimekuwa zikiendelea. Mombasa na Malindi imekuwa ikishuhudia kupotea kwa umeme mara kwa mara.

*Na Wachira Mwangi*

MANDERA

## Wapigakura wengi wanahama -IEBC

**IDADI** ya juu ya wapigakura waliotuma maombi ya kuhama kutoka kituo kimoja hadi kingine katika Kaunti ya Mandera, imeshangaza Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC).

Jana IEBC ilisema kuwa wapigakura 5,145 wametuma maombi ya kuhamisha majina yao kutoka wadi moja hadi nyingine katika kaunti hiyo tangu wiki iliyopita. Meneja wa Uchaguzi wa IEBC, Maro Ade jana alisema tayari tume hiyo imesajili wapigakura 9,837 kuanzia Oktoba 4, mwaka huu.

Eneobunge la Banisa linaongoza kwa idadi kubwa ya wapigakura waliotuma maombi ya kuhamia vituo vipya vya kura katika Uchaguzi Mkuu ujao. Wapigakura 1,010 wa eneobunge hilo wametuma maombi ya kuhamia.

*Na Manase Otsialo*

NAIROBI

## Ruto aahirisha kikao cha wawaniaji wa Bonde la Ufa

**NAIBU** Rais William Ruto jana aliahirisha ghafla mkutano aliokuwa amepanga kufanya na wawaniaji kutoka kaunti 10 za eneo la Bonde la Ufa, wanaotafuta tiketi ya chama cha UDA katika uchaguzi mkuu ujao.

Mkutano huo ulikuwa umeratibiwa kufanyika Jumanne ijayo katika makazi yake, mtaani Karen, jijini Nairobi. Dkt Ruto amekuwa akitumia makazi hayo kukutana na jumbe tofauti zinazomtembelea kutoka sehemu kwingi nchini. Tangazo hilo lilitolewa Alhamisi na Katibu Mkuu wa chama hicho, Bi Veronicah Maina.

"Chama kimetangaza kuahirishwa kwa mkutano ambao ulikuwa umepangiwa kufanyika Oktoba 26."

*Na Vitalis Kimutai*

BUNGOMA

## Mwanafunzi aokolewa akijaribu kujiua kwa kukosa karo

**MWANAFUNZI** wa Kidato cha Tatu katika shule moja katika eneobunge la Webuye Mashariki, Kaunti ya Bungoma, alinusurika kifo baada ya kuokolewa na wasamaria wema alipokuwa akijaribu kujinyonga kwa kukosa karo.

Mwanafunzi huyo ambaye amekuwa akirejeshwa nyumbani mara kwa mara kutokana na ukosefu wa karo, alichukua kamba na kuelekea katika msitu wa Chetambe kwa lengo la kujinyonga, Alhamisi jioni.

Mzee wa kijiji cha Satellite, Nathan Nyongesa, aliambia *Taifa Leo* kuwa mwanafunzi huyo alionwa na mchungaji wa mifugo alipokuwa akijaribu kujitia kitanzi.

Mchungaji huyo alipiga kamsa halafu watu wakajitokeza na kumuokoa kabla ya kujitoa roho. Kulingana na Bw Nyongesa, mama wa msichana huyo anafanya kazi katika duka la urembo ambapo anajipatia pato dogo la kijungu jikoni tu.

Mwanafunzi huyo ambaye baadaye alisema kuwa analenga kuwa daktari katika siku za usoni, alisema alilenga kujitoa roho baada ya kubaini kuwa uwezekano wa kutimiza ndoto yake ulikuwa finyu mno.

"Mama yangu ameniambia kukaa nyumbani hadi siku ambayo atapata karo. Kuna haja gani kuishi ilhali wenzangu wanaendelea na masomo yao nami nikitatizika" akasema.

*Na Brian Ojamaa*

**Ukiwa na suala lolote ungetaka kuwasilisha kwetu, tuma sms bila malipo kwa 20684 ukianza na neno 'Taifa'**